

Kilimo cha mitende katika jangwa

Tende ni mti wa matunda wa kudumu na ni maarufu sana Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati. Tende ni tunda la mawe ikimaanisha ni mbegu moja iliyozungukwa na tunda lingine lenye nyama. Tende huwa laini ikiwa kavu, na ni tamu sana.

Kukuza mitende

Kabla ya kupanda mitende, tunahitaji kwanza kuandaa miche. Ikiwa mitende itapandwa kwa idadi kubwa na usawa unahitajika, miche ya mitende inaweza kupatikana kwa njia maaalum. Miche inahitaji kufikia ukubwa fulani kabla ya kupandikizwa.

Wakati miche iko tayari, miche inaweza kupandikizwa na kupandwa kwa umbali wa mita 1.5 kati ya miti.

Hakikisha kuwa una chanzo cha maji ambacho unaweza kupata maji kwa ajili ya umwagiliaji hasa mitende ikiwa inakuzwa katika maeneo kame.

Mitende ni miti ya kudumu na huchukua takriban miaka 2 kuanza kutoa matunda.

Uchavushaji wa mitende

Ili mitende kutoa matunda, uchavushaji unahitaji kufanywa.

Uchavushaji hufanywa kwa kuhamisha chavua kutoka ua moja la dume hadi ua la kike la mimea 2 tofauti.

Chavua itakusanya kutoka kwa maua ya kiume na kuchujwa ili kutayarisha mchakato wa uchavushaji.

Kisha chavua hutumika kuchavusha mimea ya kike.

Kwa vile umuhimu wa mitende dume ni uchavushaji tu, wakulima hawapendelei kuipanda, na hivyo kupata chavua kutoka kwa wakulima wengine.

Uvunaji wa tende

Baada ya uchavushaji, matunda hukua ndani ya mwezi 1 na yanaweza kuvunwa kulingana na mahitaji ya soko. Wengine wanaweza kuvuna matunda yakiwa hayajakomaa huku wengine wakivuna matunda yakiwa yamekomaa na kuiva.

Baada ya kuvuna, tende hukaushwa na kisha huchambuliwa